Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا اله الا الله محمد رسول الله

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa mwongozo kwa watu, na Ishara zilizo wazi za mwongozo na kipambanuzi. Basi miongoni mwenu atakayeuona mwezi, afunge saumu, na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Allah Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito, na pia (Huwatakieni) mtimize hesabu na kumtukuza Allah kwa kuwa Amewaongozeni, na ili mpate kushukuru. (Al Baqarah 2:186)

JUZU 79 No. 204 | SHAB.-RAMADH. 1439 AH | MEI 2019 | HIJRAT 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Miaka 111 ya Ukhalifa

Kalenda ya Jamaat Ahmadiyya inagawanywa kwa idadi ya siku ambazo husherehekewa, au hasa huadhimishwa, duniani kote.

Siku ya Ukhalifa ni moja ya siku hizo ambayo hubeba umuhimu mkubwa zaidi. **Ukhalifa** ni kiungo ambacho huunganisha Jumuiya nzima pamoja na kuifanya kuwa moja; kitofautishi baina ya jumuiya na halaiki.

Siku hii huadhimishwa tarehe 27 Mei kila mwaka katika Jamaat zote ulimwenguni. Uadhimishaji au usherehekeaji, katika muktadha wa Jamaat, humaanisha ukumbukaji wa baraka za Allah katika suala hilo husika na kutazama namna tunavyoweza kufaidika nalo zaidi. Hayo hayo hulengwa inaposherehekewa **siku ya Ukhalifa**; Waahmadiyya humshukuru Allah kwa baraka za umoja, kwa kiungo kinachotuunganisha jumuiya



nzima pamoja kama moja na kumuahidi Allah kwamba hatutazembea na kuiacha baraka hii kubwa inayotufanya kuwa "Al-Jamaat" [Jumuiya] kama ilivyotabiriwa na Mtukufu Mtume wa Islam, rehema na Amani ziwe juu yake.

Kwa kuiadhimisha siku hii, kila tawi hufanya mikutano ambapo hotuba hutolewa. Hotuba hutawala mada mbalimbali juu ya Ukhalifa kutoka kwenye Qur'an, Hadith, maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na ushuhuda wa kihistoria juu ya namna Allah Mwenye adhama alivyo katika upande wa ***Khilafat Ahmadiyya*** mara zote.

Wahutubu wa mikutano hii huwakumbusha wahudhuriaji majaribu na adha iliyoikumba Jamaat na namna Jamaat ilivyonasuka katika magharika hayo na kuibuka mshindi, pekee na kwa sababu tu ya uongozi wa Kiungu uitwao **Ukhalifa**. Mtu anaweza jiuliza kwa nini siku isherehekewe kwa ajili ya hili? Haswa, dunia nzima hufanya hivyo. Masuala ambayo hupewa umuhimu mkubwa katika Maisha yetu hupangiwa siku; Siku ya Afya Duniani, Siku ya Wafanyakazi, Siku ya Wanawake, Siku ya Kina Baba, Siku ya Mazingira, kwa kuzitaja chache. Vipindi vya luninga, Makala za magazetini, matoleo maalum ya majarida hurasimishwa

Endelea uk. 2

Ijtimaa ya Pili ya Waqfe e Nau Yafana



Na **Idara ya Waqf Nau**.

Waahmadiyya walio katika mpango maalum wa kujitolea maisha yao katika kuitumika Islam (Waqf Nau) walifanya Ijtmaa yao iliyofanyika tarehe 19-21 ya mwezi Aprili, 2019 katika viunga vya Jumuiya Ahmadiyya vilivyopo kitonga, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Ijtmaa hiyo ya pili katika historia ya mpango huo hapa Tanzania ilianza kwa kuwashirikisha kwa pamoja kuangalia na kusikiliza hotuba ya Sala ya Ijumaa ya Khalifa Mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba].

Mashindano mbalimbali ya kielimu ikiwa ni pamoja na usomaji wa Qur'an Tukufu, Hifdhul Qur'an, Hadithi za Mtume Muhammad[saw], taratibu za sala ya Kiislam na Dua za Mtume Muhammad[saw].

Washiriki wa Ijtimaa hiyo pia walipata fursa ya kutembelea maonyesho ya wanyama na kujifunza mambo mbalimbali ya wanyama.

Ilihitimishwa kwa utoaji wa zawadi kwa washindi na nasaha za Amir Jamaat Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry.

Tukio la Kihistoria:

Khalifa Ahamia Islamabad



Na **Pazi Mazongera**

Historia imeandikwa wakati Kiongozi wa wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya duniani, Khalifa wa tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alipoondoka Masjid Fazl mara baada ya saa 12 jioni na kuelekea moja kwa moja Islamabad ambako aliwasili saa 12 na dakika 55 na kupokewa na mamia ya Waislam wa Jumuiya ya Ahmadiyya, wake kwa waume, watoto na wazee, wote hao walifurahia kumpokea Kiongozi wao mpendwa wa kiroho katika makao mapya.

Alipowasili, Khalifa Mtukufu aliwasalimia waumini hao na kuwapongeza kwa shairi zuri lililosomwa na watoto ambalo lilimshukuru Allah. Lilikuwa tukio maalum na la aina yake katika historia ya Jumuiya. Baadaye aliongoza sala ya Magharibi na Ishaa katika msikiti mpya uliojengwa

Endelea uk. 5

Ndoa ya Mtume[saw] na Bi Hafsah[ra] uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

USULI WA SIKU YA UKHALIFA

Wengi wetu tunakuwa tukisherehekea siku ya Ukhalifa Tarehe 27 Mei katika maisha yetu yote kiasi hiki ya kwamba ni tukio ambalo hatuchukui muhula kutafakari ni lini na kwanini siku hii ilianzishwa.

Siku hii ya Ukhalifa haikuwepo siku zote, ila ilianzishwa kwa mara ya kwanza tarehe 27 Mei 1957. Al Musleh -ul-Maud, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad^{ra} alifanya juhudi zote za kuifanya Jamaat itambue baraka, daraja na umuhimu wa Ukhalifa wa Kiahmadiyya.

Alipita katika wakati mgumu na wenye mawimbi makali, maadui wa Jamaat walipokuwa wamedhamiria kutokomeza Ukhalifa kwani hiyo ndiyo ilikuwa njia pekee ya kuangamiza na kubomoa nyumba iitwayo Ahmadiyyat.

Tangu Ukhalifa wa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad^{ra} mwaka 1914 hadi 1965 mashambulizi kadhaa yalifanywa dhidi ya taasisi ya Khilafat Ahmadiyya.

Allah Mwenye Nguvu daima Alilinda taasisi hii ya baraka ambayo ilianzishwa kwa amri Yake.

Ulinzi wake maalum ukasambaratisha hujuma na njama zote. Hata hivyo Khalifatul Masih wa II^{ra} aliona ni muhimu wanajamaat waelewe taasisi hii muhimu lakini pia watoe shukurani kwa neema hii kutoka kwa Allah.

Ni mwaka 1956 wakati Khuddam-ul-Ahmadiyya walipokuwa na Ijtimaa yao ya taifa mjini Rabwah ambapo walipata baraka ya kuhudhuria kwa Khalifa Mtukufu. Akiwahutubia, Khalifatul Masih wa II^{ra} aliwaambia "Daima kumbukeni neema za Ukhalifa. Kwa kulikumbuka jambo fulani, mataifa yameteuwa siku fulani kwa ajili ya kumbukumbu. Mathalan, Mashia mara moja kwa mwaka huandamana mitaani ili kwamba mauaji ya Hazrat Imam Husseinyasisahaulike. Hivyohivyoninawashauri Khuddam siku moja kusherehekea Ukhalifa ambapo watatoa shukrani zao kwa Allah na hivyo kuhuisha historia. Yaweza kuwa vigumu kuyapata magazeti ya zamani lakini *Al Fazl* hivi karibuni imeeleza historia nzima. Hoja za Khalifatul Masih wa I^{ra} za kuunga mkono Ukhalifa na jinsi alivyotukanwa na Paighamis [Ahmadiyya Anjumani - Ishaat-i-Islam Lahore, ambao walitoka kwenye nidhamu ya Ukhalifa].

"Makala hizo zisomwe kutoka kwenye magazeti haya. Kama siku ya Ukhalifa inaazimishwa kila mwaka, vijana watasikiliza makala hizo na hatimaye watazihifadhi kwa ghaibu. Endeleeni kufanya mikutano hii mpaka siku ya kiyama, ili Jumuiya isisahau neema, baraka na umuhimu wa Ukhalifa.

Ukhalifa wa Issa^{as} umekuwepo kwa miaka 1900. Tunaomba Ukhalifa wa Masihi Aliyeahidiwa^{as} ambaye ana cheo kuliko Issa^{as} uendelee kwa miaka 10,000. Hii inawezekana tu mkiwa na siku maalum ambayo mmepanga kwa dhumuni hili.

"Ningependa pia kuagiza Makao Makuu kuwa, kama tulivyo na siku ya ***Sirat-un-Nabi***, tuwe na siku ya kusherehekea siku ya Ukhalifa. Makao makuu iwashauri [waandaaji wa mikutano hii] mada zipi za kuzungumzia, sehemu ipi ya *Al Fazl* ya kuwasomea vijana wetu ili watambue Khalifatul Masih wa I^{ra} alivyouhami Ukhalifa na jinsi Paighami walivyoleta upinzani. Njozi hizo na kashf nilizopatiwa na Allah mapema zitajwe na kuoneshwa zilivyotimia na Allah Kuonesha kuwa baraka Zake ziko kwa Ukhalifa."

Kwa mnasaba wa maagizo hayo ya Khalifatul Masih II^{ra}, Nazarat Islah o Irshad, kwa kushauriana na wanajamaat walishauri kuwa tarehe 27 Mei iwe siku ya Ukhalifa itakayoadhimishwa na Jamaat zote. Tangazo hili lilitoka katika gazeti la *Al Fazl* la tarehe 9 Novemba 1956.

Toka wakati huo Jamaat Ahmadiyya inasherehekea baraka za Ukhalifa siku hiyo, husherehekea kwa maombi, kukumbuka neema za Allah kwa Jamaat ambazo zote hizo zinatokana na taasisi hii ya baraka, na kutizama jinsi kila mwaka unaopita unavyoleta maendeleo kwa Jamaat chini ya uongozi huu wa kimbingu.

Rai za Mwana Aliyeahidiwa^{as} Juu ya Miiko ya Saumu

Maktaba Yetu

SAUMU KWA WATOTO

Wako watu wengi ambao huwafanya hata watoto wadogo wafunge saumu ya Ramadhani, ilhali kila faradhi na agizo huwa linakuwa na mpaka na wakati tofauti. Kwa rai yetu baadhi ya hukumu huanza kutekelezwa na mtoto mwenye umri wa miaka minne. Wakati baadhi ya maagizo huanza kutekelezwa na mtoto mwenye umri wa miaka saba hadi kumi na mbili. Na baadhi ya sharia huanza kutekelezwa na mvulana mwenye umri kuanzia miaka kumi na tano au kumi na nane.

Kwa rai yangu agizo la kufunga saumu linamhusu mvulana au msichana wa kuanzia miaka kumi na tano hadi kumi na nane. Kwa sababu huu ndio umri wa kubalehe kwa vijana wengi sana. Mtoto aanze kujengwa tabia ya kufunga saumu wakati akiwa na umri wa miaka kumi na tano. Na anapokuwa na umri wa miaka kumi na nane basi ni faradhi kwake kufunga saumu ya Ramadhan.

"Mtoto atakapofika umri ambao atakuwa na nguvu ya kutosha kufunga, yaani umri wa miaka kumi na tano, basi hapo ndipo aagizwe kufunga hatua kwa hatua. Mwaka wa kwanza afanye kadri atakavyoweza (si lazima amalize mwezi mzima). Mwaka wa pili afunge siku nyingi zaidi kuliko mwaka uliopita. Na mwaka wa tatu afunge zaidi ya miaka iliyopita. Kwa njia hii atazoezwa kuwa mwenye kufunga saumu." (*Al Fazl* ya tarehe 11 - 4 - 1925).

WAGONJWA NA WASAFIRI

Kwa upande wa wagonjwa na wasafiri, Mtukufu khalifa wa pili (r.a) alisema:

"Yule mtu anayefunga saumu ya Ramadhan akiwa mgonjwa au safarini, basi yeye ameasi wazi wazi kabisa agizo la Mwenyezi Mungu. Kwani Mwenyezi Mungu. Kwani Mwenyezi Mungu ameeleza wazi wazi kabisa kwamba mgonjwa na msafiri wasifunge saumu ya Ramadhan. Angeweza kufunga baada ya kupona. Au angeweza kufunga akifika mwisho wa safari yake."

"Ni lazima kutekeleza agizo hili kwa sababu wokovu hupatikana tu kwa Fadhili za Allah. Hakuna mtu anayeonyesha vitendo vyake vya kutumia mbavu. Mwenyezi Mungu Hakusema kuwa ikiwa maradhi yatakuwa makubwa au madogo. Hakusema ikiwa safari itakuwa fupi au ndefu. Bali ni kuwa agizo la kawaida halina mpaka. Ni lazima litekelezwe jinsi lilivyo. Ikiwa mgonjwa au msafiri atafunga, basi fatwa ya kumwasi Allah itapigwa juu yake." (*Al-Badr* 17 - 10 - 1907).

Miaka 111 ya Ukhalifa

Kutoka uk. 1

mahsusi kwa sababu ya hiyo siku iliyoadhimishwa. Hii husaidia kulipa umuhimu suala lililopo mkononi na kuuzindua umma. Ni hivi karibuni tu dunia imeanza kutenga siku kwa ajili ya madhumuni maalum, ambapo Qur'an Tukufu imetuelekeza kufanya hivyo kabla ya yeyote kufikiria hivyo. "***Zakkirhum bi Ayyamillah***" ni amri ya Qur'an, inayomaanisha, "na uwakumbushe siku za Allah". Hivyo kwa kuziadhimisha siku hizo, tunafuata amri ya Qur'an Tukufu.

Ikumbukwe pia kwamba tunaadhimisha siku hizi kwa sababu hii tu ya kujikumbusha sisi wenyewe na vizazi vyetu juu ya ishara na baraka za Allah. Hakuna siku katika kalenda ya Jamaat iliyopangiwa siku za kuzaliwa wala kumbukizi za vifo, badala yake siku hizo hupangwa kuzisherehekea ishara za Allah.

Siku ya Masihi Aliyeahidiwa (23 Machi) huadhimishwa kutimia kwa bishara ya Mtukufu Mtume^{saw} ya kwamba Masihi atakuja kuiokoa dunia siku za mwishoni. **Siku ya Mwana Aliyeahidiwa** (20 Februari) huadhimisha utimilifu wa bishara ya Masihi Aliyeahidiwa^{as} ya kwamba Allah Atainua miongoni mwa kizazi chake mhuishaji ambaye ataupeleka ujumbe wa Islam kwenye kona za dunia.

Mtafaruku uliotokea baina ya makundi mawili wakati wa uchaguzi wa Hadhrat Khalifatul Masih II^{ra} lazima pia ukumbukwe inapoadhimishwa siku ya Ukhalifa. Kulitokea fikra bandia wakati ule ya kwamba hakukuwa na haja ya Ukhalifa katika Jamaat na kwamba Sadr Anjuman Ahmadiyya alitosheleza kuendesha masuala ya Jumuiya.

Wakati kundi kubwa la Jumuiya linafikiria vinginevyo – kwamba lazima uwepo Ukhalifa, la sivyo mfumo mzima utaanguka – watetezi wa kundi la kupinga Ukhalifa walikuwa watu wenye elimu kubwa, mashuhuri sana, wenye viwango vya elimu vitambulikavyo duniani, juu ya yote, walikuwa wasimamizi wa mali za Jumuiya. Wakaamua kujigawa na kuondoka na mali zote za Jumuiya.

Ilionekana kama pengo kubwa sana, lakini Hadhrat Khalifatul Masih II^{ra} – licha ya kuwa mdogo kiumri na bila ya mali yoyote – hakukodolea macho katika masurufu ya kidunia kama njia ya kuielekea shabaha kubwa ya kiroho. Aliamini kwamba ilikuwa ni Jumuiya ya Allah na Allah Pekee alikuwa Anaitosheleza. Ilikuwa ni suala la muda tu kuthibitisha kwamba wale waliokimbia na masurufu ya kidunia yatawatindikia ndani ya miongo michache wakati Jumuiya – "Al Jamaat" ya Mtukufu Mtume^{saw} na Masihi Aliyeahidiwa^{as} – kuendelea kunyeshelezewa kila baraka (ya kidunia na kiroho) na mafanikio ambayo yamedumu kwa zaidi ya karne na robo, na yanaendelea.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Ndoa ya Mtume[saw] na Bi Hafsah[ra]

Na Mwl Abdullah H. Mbanga

Miongoni mwa ndoa za Mtume[saw] zinazoshutumiwa za Mtume[saw], ni ndoa yake na Hadhrat Hafsah[ra]. Hapa tunaeleza hadithi nzima ya ndoa hiyo ili kubatilisha madai ya wakosoaji wa ndoa hii, ambao bila shaka wako gizani kuhusu hadithi nzima ya ndoa hii.

Hadhrat Hafsah alikuwa ni binti wa Hadhrat Umar ibn Khattab Al Faruq[ra], aliyekuwa sahaba wa karibu mno wa Mtume[saw]. Ambaye baadaye alikuja kuwa Khalifa wa pili wa Mtume Mtukufu[saw].

Mjomba wake Hafsah, Hadhrat Uthman ibn Maz'un, pia alikuwa ni miongoni mwa masahaba maarufu wa Mtume[saw]. Baba mdogo wa Hafsah, Zaid ibn Khattab naye alikuwa Sahaba.

Abdullah ibn Umar[ra], alikuwa sahaba na mpokezi maarufu wa hadithi, huyu alikuwa ni kaka wa Hafsah.

Kimaumbile Hafsah alikuwa ni mwanamke wa kawaida wa Kiarabu, lakini kikhulka alikuwa mwanamke mcha Mungu mno. Mikono yake ilibeba kipaji cha hali ya juu cha uandishi. Kinywa chake kilijaaaliwa ufasaha wa maneno, alikuwa mmojawapo wa wanawake mabingwa wa kujieleza na wenye vipawa vikubwa vya kujenga hoja.

Hata Hadhrat Aisha[ra], mke mwingine wa Mtume Mtukufu[saw], ambaye Mtume[saw] ametutaka tujifunze nusu ya elimu ya dini kutoka kwake, aliwahi kusema kwamba mara nyingi alikuwa akimchukulia Hafsah kuwa kama mfano mwema kwa ajili yake.

Kaika kitabu kiitwacho *Mustadrakul Hakiim* jz 4 uk, 15, imeelezwa kuwa; siku moja Mtume[saw] aliwahi kutokewa na Malaika Jibril na kuambiwa juu ya Hadrat Hafsah kuwa, Ni mwanamke anayefunga na kusali mara kwa mara na peponi pia atakuwa mke wako.

Hafsa alipotimu hirimu ya kuolewa, mume wake kwanza alikuwa ni Hadhrat Khanis ibn Huthafah Al Sahmi[ra], ambaye alijiunga na Uislam kwa mkono wa Abu Bakr[ra].

Kutokana na mateso yaliyokuwa yakiwakumba Waislam katika Makka, Hadhrat Khanis ibn Huthafah na mkewe Bi Hafsah waliamua kuhamia Madina. Huko walikaribishwa katika nyumba ya Hadhrat Rafa'h bin Abdul Munthir.

Wanandoa hao walifurahia sana maisha ya Madinah na hasa kuwa miongoni mwa muhajiriin. Hafsah[ra] alianza mpango wa kuhifadhi aya za Kur ani Tukufu kila zilipokuwa zikiteremka. Kisha alikuwa akifanya tafakuri ya kina juu ya maana zake za ndani.

Kwa upande wake, mumewe alikuwa akijibidiisha katika mazoezi na mafuzo ya upambanaji kwa ajili ya ulinzi wa Islam. Maana wakati huo kulikuwa na tishio kubwa la kuvamiwa na watu wa Makka.

Ndipo ghafla zikatangaa habari kwamba jeshi kubwa la makureshi wa Makka liko njiani kuelekea Madina chini ya uongozi wa Abu Jahl. Lengo kuu likiwa ni kuisambaratisha dini tukufu ya Islam.

Hadhrat Khanis ibn Huthafah alipopata habari hii, alipandwa na mori mkubwa wa mapambano. Aliapa kuipigania Islam hadi tone la mwisho la damu yake. Hamu yake kubwa ilikuwa ni kulidhalilisha vilivyo jeshi la Abu Jahl.

Jeshi la Waislam liliweka kambi katika mji wa Badr, walikuwa wachache na dhaifu, hali kadhalika walikuwa na silaha duni mno.

Walichofanya ni kudhibiti chanzo pekee cha maji katika eneo hilo, kisha wakatawakali juu ya Allah.

Vita ya Badr ilikuwa ni vita ngumu sana kwa Waislam. Walikuwa na jeshi lenye watu 313 wasiokuwa na silaha yoyote ya maana, lakini walikuwa katika makabiliano na jeshi la watu takriban 1000, wenye mafunzo makubwa na silaha za kisasa kwa zama hizo.

Katika historia ya dunia ghazwatul Badr ni mojawapo ya vita kubwa zilizowahi kupiganwa, ambapo kundi la watu wachache wenye silaha hafifu, walilisambaratisha jeshi kubwa lenye silaha bora.

Mume wa Hadhrat Hafsah, Khanis ibn Huthafah, Baba yake Hafsah Umar ibn Khatab na ami yake Hafsah Zaid ibn Khattab, wote walishiriki katika vita hii muhimu katika historia ya Islam.

Vita viliposhika kasi Khanis alijitoma katikati ya jeshi la makafiri wa Makka. Alitembeza kichapo cha nguvu dhidi ya makafiri hao kwa kutumia jambia lake.

Inasimuliwa kuwa Khanis alifanikiwa kupunguza idadi kubwa ya wanajeshi wa kikureshi, hali hii ilidhoofisha vibaya jeshi hilo ambalo hatimaye lilipoteza pambano. Makamanda wengi wa jeshi hilo waliuawa. Lakini Khanis ibn Huthafah alijeruhiwa vibaya mno.

Waliporudi nyumbani na ushindi, Hadhrat Hafsa alifurahi mno. Furaha yake iliongezeka zaidi aliposikia watu wakizungumzia ushujaa aliounyesha ibn Huthafah katika vita hivyo.

Alipobaini kuwa mumewe yu katika hali mbaya ya majeraha. Hadhrat Hafsah[ra] alihisi kuwa anahitajika kumhudumia mumewe kimatibabu, jambo hili lilikuwa jukumu zito lililohitaji juhudi kubwa. Basi ghafla akasoma ile aya iliyopo katika Suratul Anfaal iliyoteremshwa kuhusiana na vita hiyo ya Badr isemayo;;

Wa maa ja'lahu llahu illaa bushraa wa litatma-inna quluubukum, wa ma al nasru illa min 'indillahi. Innallaha 'aziizun hakiim.

Na Allah hakufanya haya ila iwe habari ya furaha na ili mioyo yenu itulie kwayo. Na hakuna msaada ila utokao kwa Allah, hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hakima. (8:11)

Aya hii ilimtia hamasa kubwa katika jukumu zito la kumuuguza mumewe na kuhakikisha kuwa anarejea katika afya yake ya zamani. Hili halikuwezekana, waswahili wanasema kuwa Allah alimpenda zaidi. Khanis ibn Huthafah[ra], alipoteza maisha siku chache baadaye na kuingia katika orodha ya mashahidi wa Badr.

Hadhrat Hafsah[ra] alihuzunishwa sana na msiba huu. Katika kupambana na huzuni hiyo Hafsah alizidisha mno ibada. Alikuwa akisali sala nyingi za nafali na kufunga saumu akimuomba Mola wake ampe subira katika kipindi hicho kigumu. Wakati huo Hafsah alikuwa bado msichana, umri wake ulikuwa ni miaka 21 tu.

Hafsah aliyekuwa mzungumzaji hodari, ghafla akabadilika na kuwa mkimya mno na kutwa alishinda ndani.

Hali hii ilimuumiza sana baba yake, Hadhrat Umar ibn Khattab[ra]. Uvumilivu wake, ucha Mungu wake na uelewa wake wa Qur'an Tukufu, yalikuwa ni mambo ya kupendeza. Lakini upweke uliomsibu ghafla ulimfanya baba yake achukue hatua kwa kuhofu upweke huo usije kuwa ndiyo sehemu iliyobaki ya maisha yake.

Ndipo alipoamua kumuendea Hadhrat Uthman bin Affan[ra], aliyekuwa amefiwa na mkewe Ruqaiya, binti wa Mtume[saw]. Umar[ra] alihisi kwamba kwa kuwa Hadhrat Uthman amepoteza mke na Hadhrat Hafsah amepoteza mume, basi wawili hawa wanafanana kihali, hivyo aliona ni vyema wakaoana ili iwe nafasi ya kila mmoja wao kujiliwaza na msiba uliomkuta.

Lakini Hadhrat Uthman alipopewa ushauri huu hakutoa jibu lolote. Aliinamisha uso wake na kupiga kimya cha muda mfupi. Baadaye akasema kuwa alihitaji muda kufikiria suala hilo.

Hadhrat Umar alimwendea tena Uthman baada ya siku kadhaa na kumuuliza iwapo ameshafikiria na kupata jibu juu ya pendekezo hilo. Hapo Hadhrat Uthman akajibu kuwa hakuwa na mpango wa kufanya ndoa kwa wakati ule.

Ndipo Hadhrat Umar[ra] akamwendea Hadhrat Abu Bakr[ra] na kumpa pendekezo la kumuoa binti huyo. Abu Bakr pia aliinama tu, na hakujibu chochote.

Hadhrat Umar akaingiwa na hofu kubwa juu ya mustakbali wa maisha ya binti yake. Maana wote aliowakabili na kuwataka wamuoe walilikataa pendekezo lake. Alitaraji kuwa ombi lake lingepokelewa kwa shauku na furaha, lakini hali ilikwenda kunyume na matarajio yake. Watu aliowategemea mno katika udugu wa imani, ambao alitamani waunge naye udugu zaidi kupitia ndoa, katika hali ya kusikitisha mno hawakuwa tayari kuupokea udugu huo, aliwaza.

Ndipo sasa akaamua kumkabili Mtume[saw] na kumshitakia juu ya hali iliyomkuta. Alimweleza suala hili Mtume[saw] huku akiwa na hali ya huzuni kubwa mno. Kiasi cha kumfanya Mtume Mtukufu Muhammad[saw] abaini kuwa suala hili limemchangaya Hadhrat Umar[ra].

Baada ya Hadhrat Umar kuhitimisha maelezo yake, Mtume[saw] akamwambia huku akiwa ametabasamu kwamba asihofu wala kuhuzunika, kwani Allah akipenda atampatia Hafsah mume bora kuliko Uthman, na inshallah, Uthman naye atapata mke bora kuliko Hafsah.

Hadhrat Umar alifurahi sana kusikia kauli hii ya Mtume Mtukufu[saw]. Lakini akajiuliza, ni nani huyo atakayekuwa mume bora wa Hafsah kuliko Uthman?

Siku chache baadaye Mtume[saw] akamuozesha binti yake Ummu Kulthum kwa Hadhrat Uthman[ra]. Hapo akabaini kutimia kwa sehemu ya kwanza ya usemi wa Mtume[saw]. Lakini akabaki na shauku ya kutimia kwa usemi wa pili, ambao ulimhusu binti yake Hafsah. Aliendelea kujiuliza nani huyo aliye mbora kuliko Uthman!

Ndipo baadaye Mtume[saw] akapeleka posa kwa ajili ya Hafsah[ra].

Hadhrat Umar[ra] hakuamini masikio yake, kwamba eti binti yake ataingia katika kundi la mama wa waaminio ambapo wakati huo walikuwa ni Hadhrat Aisha bint Abu Bakr na Hadhrat Sadudah bint Zama'ah.

Ndipo Hafsah akaolewa na

Endelea uk. 4

Ndoa ya Mtume^{saw} na Bi Hafsah^{ra}

Kutoka uk. 3

Mtume^{saw} katika mwaka wa tatu Hijria kabla ya vita vya Uhud. Wakati huo Hafsah alikuwa na umri wa miaka 22.

Kwa tukio hili, ile kiu ya Hadhrat Umar ya kushuhudia utimilifu wa kauli ya Mtume^{saw} juu ya Hafsah kupata mume bora kuliko Uthman ikawa imekatwa kikamilifu.

Kwa jazba ya furaha, Umar^{ra} alijikuta akikariri kipande cha aya ya Qur'an Tukufu kisemacho;

Hadhaa min fadhwli rabbii,liyabluwanii a-ashkur am akfur. Faman shakara fainnamaa yashkuru linafsihii, wa man kafara fa-inna rabbii ghaniyyun kariim.

Haya ni kwa fadhili za Mola wangu ili Anijaribu iwapo nitashukuru au nitakufuru? Na anayeshukuru, basi anashukuru kwa ajili ya nafsi yake tu; na anayekufuru, kwa hakika Mola wangu ni Mkwasi, Mkarimu. *(27:41)*

Baada ya kuingia katika ndoa na Mtume^{saw}, Hadhrat Hafsah^{ra} alithibitisha kwa nini alifaa kuwa mke wa Mtume wa Allah. Alikuwa na kichwa chepesi mno kuhifadhi aya za Qur'an Tukufu kila zilipoteremka. Si hivyo tu bali pia alitumia muda mwingi kutafakari maana zake za ndani, na mara kwa mara alikuwa akijadili na Mtume Mtukufu^{saw} katika hali ya kujifunza elimu na hekima zilizomo katika aya hizo.

Pia alikuwa mdadisi mkubwa katika mambo mbalimbali yaliyohusu sheria za kiislam.

Jabir bin Abdullah Ansari, anasimulia kisa alichosimuliwa na Ummu Mubashar, mmoja wa masahaba wa kike wa Mtume Mtukufu wa Islam. Inasemwa kuwa siku moja Ummu Mubashar, Hafsah na Mtume^{saw} walikuwa wameketi mahala wakizungumza.

Ndipo Mtume^{saw} akasema kuwa watu wote waliofanya baiat chini ya mti kule, wataingia peponi bila ya kugusa moto. Hapo Hadhrat Hafsah akahopji, hilo litawezekana vipi? Swali hili lilimkera Mtume^{saw}, lakini Hafsah hakukoma bali aliendelea kutilia nguvu hoja yake kwa kunukuu aya ya Qur'an Tukufu izungumzayo juu ya moto kwamba;

Wa im minkum illaa waariduhaa, kaana 'alaa rabbika hatmam maqdhwiyyan.

Wala hakuna ye yote katika ninyi ila ni mwenye kuifikia. Ndiyo wajibu juu ya Mola wako uliokwisha hukumiwa. (19:72)

Mtume^{saw} akijibu hoja hii, naye alinukuu aya iliyofuatia isemayo; *Thumma nunajjiil ladhiinat taquu wa nadharudh dhwaalimiina fiihaa jithiyyan.*

Kisha Tutawaokoa wale wamchao (Allah); na Tutawaacha wadhalimu humo wakiangukia magoti. (19:73)

Miongoni mwa wakeze Mtume^{saw}, waliotokana na kabila la kikuresh ni wanne tu. Ummu Habibah, Aisha, Saudah na Hafsah. Hawa japokuwa alikuwa wake wenza lakini walikuwa marafiki wenye ushirikiano wa hali ya juu.

Desturi ya Mtume^{saw} ilikuwa kwamba kila baada ya sala ya asr, alikuwa akiwatembelea wakeze wote kwa zamu, akiwatakia hali na kuzungumza nao kwa muda, kuona kama kuna shida au mahitaji yoyote na kuwatekelezea. Hii ilikuwa ndiyo ratiba yake ya kila siku. Kila mke alikuwa akiisubiri ratiba hii kwa hamu kubwa.

Kuna kipindi, Mtume^{saw} alionekana kutumia muda mrefu zaidi kwa Hadhrat Zainab bint Jahsh^{ra}. Jambo hili lilikuwa likimkera Hadhrat Aishah^{ra}. Hivyo akawaeleza jambo hili washirika wake wakubwa, Hafsah na Saudah.

Aliwalalamikia kuwa yeye huwa na hamu sana na mumewe, hivyo inamhuzunisha mno kuona kwamba anachelewa kufika kwake kutokana na kutumia muda mwingi na Zainab.

Basi watatu hao wakaungana kuchunguza kulikoni kinachomchelewesha Mtume^{saw} kutoka katika nyumba ya Zainab. Ndipo wakagundua kuwa kuna ndugu mmoja alimletea Hadhrat Zainab aina fulani maalum ya asali. Hadhrat Zainab alikuwa akimwandalia asali hiyo Mtume^{saw} kila alipofika, na hii ikawa ndiyo sababu ya kumchelewesha Mtume^{saw} katika nyumba ile.

Jambo hili halikumfurahisha sana Aisha. Lakini kutokana na heshima aliyokuwa nayo juu ya mumewe, hakuweza kumtamkia. Hivyo alishauriana na washirika wake kwamba Mtume^{saw} atakapofika katika nyumba ya kila mmoja wao, ajifanye kwamba anasumbuliwa na harufu fulani kinywani mwa Mtume^{saw}.Basi Mtume alipopata malalamiko haya kutoka kwa wote hawa watatu, akahisi kwamba harufu hiyo huenda ikawa ni ya ile asali. Akaamua kujiharamishia asali kwa ajili ya kuondoa usumbufu kwa wake zake.

Kwa kuwa Allah alijua kwamba waumini wanaweza kumuiga Mtume^{saw} na kujiharimishia chakula hicho muhimu kabisa kiafya, basi Aliamua kumzindua Mtume wake Mtukufu kwa aya hii ya Qur'an Tukufu.

Yaa ayyuhan nabiyyu lima tuharrimu maa ahalla llahu laka tabtaghii mardhwaat azwaajika.

Ewe Nabii! mbona unaharimisha Alichokuhalalishia Allah? Unatafuta radhi ya wake zako; na Allah ni Msamehevu, Mwenye huruma. *(66:2)*

Ni katika wakati huohuo ndipo Mtume^{saw} alipata kumwambia Hadhrat Hafsah^{ra} habari fulani ya siri, na alimtafadhalisha kutomweleza mtu yeyote siri hiyo. Lakini Hadhrat Hafsah, kutokana na ukaribu na ushirika alio nao juu ya Aisha, aliamua kumnong'oneza siri hiyo kirafiki. Lakini Allah Akamjulisha Mtume wake juu ya kadhia hiyo. Akamteremshia aya ifuatayo;

Wa idh asarran nabiyyu ilaa ba'dhwi azwaajihii hadiithan, falammaa nabba-at bihii wa adhwharahullahu 'alaihi 'arrafa ba'dhwahu wa a'radhwa 'an ba'dhwin. Falammaa nabba-ahaa bihii qaalat man anba-aka haadhaa, qaala nabba-aniil 'aliimul khabiir.

Na Nabii alipomwambia mmoja wa wake zake hadithi kwa siri, basi (mke yule) alipovunja siri, na Allah Akamdhihirishia Nabii, akamjulisha sehemu yake na akaacha sehemu nyingine. Basi alipompasha (mkewe) habari hii akasema: Nani amekupa habari hii? (Nabii) akasema; Amenipa habari Aliye Mjuzi, Mwenye habari *(62:4)*

Hafsah^{ra}, alifariki mnamo mwaka wa 45 Hijria akiwa na umri wa miaka 58, amefariki akiwa katika saumu.

TANGAZO LA IJTIMAA YA 30 YA KHUDDAM-UL-AHMADIYYA TANZANIA

Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inapenda kuwataarifu Khuddam na Atfal wote nchini kuwa Ijtimaa yao ya 30 itakuwa tarehe 14-16 Juni, 2019 Kitonga, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

In-Shaa-Allah.

Khuddam na Atfal wote wanaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Limetolewa na Idara ya Isha'at ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

Muradi Hasa wa Baiat

Muradi wa Baiat ni kuikabidhi nafsi kwa Mwenyezi Mungu, mradi wake ni huu kwamba leo tumeiuza nafsi yetu kwa Mwenyezi Mungu. Hii si sahihi kabisa kwamba hatimaye mtu anaweza kupata hasara kwa kutembea katika njia ya Mwenyezi Mungu. Mkweli hawezi kamwe kupata hasara. Hasara ni ya yule aliye mwongo, avunjaye Baiat na ahadi aliyoifunga na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya dunia. Mtu yule atekelezaye mambo hayo kwa ajili tu ya kuihofia dunia, basi na akumbuke kwamba wakati wa mauti hakuna mtawala wala mfalme yeyote atakayeweza kumuokoa. Yeye ni mwenye kwenda tu kwa Hakimu wa mahakimu wote Atakayemuhoji kwamba kwa nini hukunijali? Hivyo ni muhimu kwa kila mwaminio kwamba amuamini Mwenyezi Mungu Aliye Mmiliki wa Mbingu na Ardhi na afanye toba ya kweli."

(Malfuudhaat jal. 7 uk. 29 – 30).

Ujana wa Seyidna Ahmad[as]



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

Seyyidna Ahmad[as] Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya aliishi maisha yake yote chini ya mafundisho ya Qurani Tukufu na sawa na Sunna ya mpendwa wetu Mtume Muhammad[saw] Katika makala ya leo nitajaribu kuwaelezeni baadhi ya matukio ya maisha ya ujana wake.

Sala yake :: Seyyidna Ahmad[as] Alikuwa akipenda sana kuendeleza ibada za Mwenyezi Mungu hasa sala za faradhi. Kwa niaba ya baba yake alienda kufuatilia kesi Fulani, mwenyewe anasema: "Nilikwenda Batala kufuatilia kesi moja. Saa ya sala ikafika nami nikaanza kusali. Mtumishi wa mahakama aliniita, lakini nilikuwa nikisali. Mdaiwa alihudhuria na akataka kufaidika kwa kupendelewa na akasisitiza sana jambo hili. Lakini mahakama haikujali, na kesi ilihukumiwa dhidi yao nami nikashinda kesi. Nilipomaliza sala, nikaenda, nikafikiri kwamba pengine hakimu amechukulia kisheria kutohudhuria kwangu, kwa hiyo nikasema kwamba nilikuwa nasali. Hapo yeye akasema nimekwisha amua, umeshinda kesi." (*Hayatun Nabii*, J. 1, uk. 56)

Unyenyekevu wake :: Mtumishi wake Bwana Mirza Ismaili Beg marehemu anashuhudia kwamba kabla ya kutumwa kwake, Seyyidna Ahmad[as] kwa amri ya baba yake alipokuwa akienda kumwakilisha katika kesi alikuwa na farasi pamoja naye, nami mara nyingi nilikuwa nafuatana naye. Wakati wa kuondoka, mwenyewe alikuwa akitembea na kunipandisha juu ya farasi. Nilikuwa nikiomba radhi na kusema mara kwa mara naona aibu, lakini yeye alikuwa akisema, "Sioni aibu kutembea, mbona unaona aibu kupanda."

Wakati wa kuondoka Qadian, daima alikuwa akinipandisha kwanza, na baada ya kupita karibu nusu ya umbali, nilikuwa nikishuka na yeye alikuwa akipanda. Kadhalka, wakati wa kurudi kutoka mahakamani, yeye alikuwa akinipandisha kwanza na baadaye alikuwa akipanda mwenyewe. Alipokuwa akipanda alikuwa akimwacha farasi aende kwa mwendo aendavyo." (*Al Hakam* 21/28 Mei 1934)

Hadimu wake mwingine Bwana Mirza Din Muhammad anaeleza, "Mwanzoni sikujuana na Hadhrat Masihi Mau'udi[as], yaani sikuzoea kumtembelea. Seyyidna Ahmad[as] mwenyewe alikuwa akiishi upweke, pasipo kujulikana, lakini kwa kuwa yeye alikuwa msimamizi wa sala na saumu na mwenye kupenda sheria, basi shauku hiyo hiyo ilinipeleka kwake na nilianza kukaa naye. Alipokuwa akienda kufuatilia kesi alikuwa akinipandisha juu ya farasi nyuma yake na baada ya kufika Batala alikuwa akimfunga kwenye jumba lake. Jumba hili lilikuwa na ghorofa, alikuwa akiishi humo. Mtunzaji wa nyumba hiyo alikuwa mfumaji mmoja aliyekuwa mtu maskini. Baada ya kufika huko alikuwa akiagiza chakula cha pesa mbili kwa ajili yake ambamo vipande vya robo ya chapati moja alikuwa akila na maji. Chapati iliyosalia na dengu na kadhalika iliyokuwa pamoja na chapati alikuwa akimpatia yule mfumaji. Alikuwa akinipa Anna nne kwa chakula. (Anna moja ni sawa na pesa nne.) Alikuwa anakula kidogo sana na alikuwa hana uchu wa chakula chochote. (*Hayati Ahmad[as]* jalada 2 uk. 196)

Kamwona Mtume Mtukufu[saw] :: Mnamo mwaka 1864 au 1865, wakati umri wake ulipokuwa miaka 30 au 31, yeye alimwona Mtume Mtukufu[saw] katika kashfi. Kashfi hii inafafanua upendo na mapenzi yake kwa Mtume Mtukufu[saw], Yeye anaandika:

"Mwanzoni mwa ujana wangu, usiku moja niliota kwamba nipo katika nyumba yenye shani kubwa iliyo takatifu na safi sana, humo ndani anazungumzwa na anatajwa-tajwa Mtume Mtukufu[saw] Nikawauliza watu kwamba Mtume Mtukufu[saw] amejikalia wapi? Wakaashiria kwenye chumba kimoja. Basi, pamoja na watu wengine nikaingia ndani. Nilipomwambia Hudhur[saw], yeye alifurahi sana na akanirudishia jibu la salamu yangu kwa njia bora sana. Nakumbuka mpaka sasa uzuri wake na sura yake ya kuvutia na mtazamo wake wa upole na upendo, wala siwezi kusahau. Mapenzi yake yakanivutia ajabu, na wajihi wake mzuri ukanifanya nimpende sana. Wakati huo akaniuliza: Ee Ahmad! Kuna kitu gani katika mkono wako wa kulia? Nilipoona kwenye mkono wangu wa kulia, nikaona kuna kitabu mkononi mwangu, na nikafikiria ni kitabu kilicho utungo wangu. Nikasema, Hudhur, hiki ni kitabu kilicho utungo wangu.(Tafsiri kutoka *Aina Kamalate Islam* uk. 548, 549)

Mtume Mtukufu[saw] akiona kitabu hicho akauliza kwa lugha ya Kiarabu, umekiitaje kitabu hiki? Nikajibu, nimekiita kitabu hiki Qutbi… Ilmuradi, Mtume Mtukufu[saw] alichukua kitabu kile kutoka kwangu. Kitabu kile kilipokuja tu mkononi mwa Mtume Mtukufu[saw] mara kwa kuguswa na mkono mtakatifu wake kitabu kile kikawa tunda zuri lenye rangi ya kupendeza lililoshabihiana na pera lakini saizi yake ilikuwa kama tikitimaji. Mtume Mtukufu[saw]



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as]
Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa

alipotaka kulikata vipande vipande kwa kuligawa, ilitoka asali kutoka ndani yake kiasi hiki kwamba mkono wake mtukufu ulijaa asali mpaka kiwiko. Hapo mfu mmoja aliyekuwapo nje ya mlango, kwa muujiza wa Mtume Mtukufu[saw] akihuika akaja na kusimama nyuma yangu, nami nilikuwa nimesimama mbele ya Mtume Mtukufu[saw] kama mdai anavyosimama mbele ya hakimu. Na Mtume Mtukufu[saw] alikuwa amejikalia kiti kwa jaha na taadhima na kwa shani ya hakimu kama mshindani mwereka.

Basi, kwa kifupi ni kwamba Mtume Mtukufu[saw] akanipa kipande kimoja ili nimpe mtu aliyehuika upya, na vipande vilivyosalia vyote akatia ndani ya joho langu. Kipande kile kimoja nilimpa mtu aliyehuika hivi punde, yeye akala. Basi, aliyekuwa amehuika alipokwishakula ndipo (*Barahine Ahmadiyya*, sehemu 3, uk. 248, 249, maelezo ya pembeni kwenye maelezo ya pembeni Na. 1) nikaona kwamba kiti cha Mtume Mtukufu[saw] kiliinuka sana kiasi hiki kwamba kilikaribia dari na nikaona uso wake mtakatifu ulianza kun'gaa kana kwamba miali ya jua na mwezi inauangukia. Nami nilikuwa ninatazama uso wake mtakatifu kwa shauku na mapenzi huku machozi yakinitiririkia. Kisha nikaamka na nilikuwa bado nalia. Na Mwenyezi Mungu Alinitilia moyoni mwangu kwamba mfu yule ni Islam na sasa Mwenyezi Mungu Ataihuisha kwa baraka za kiroho za Mtume Mtukufu[saw] kwa mkono wangu.

(Tafsiri kutoka '*Aina Kamalate Islam*', uk. 548-549)

Khalifa Ahamia Islamabad

Kutoka uk. 1

hivi karibuni uitwao Masjid Mubarak.

Mapema, mamia ya Waahmadiyya walimuaga Khalifa Mtukufu wakati akiondoka Masjid Fazl ambako palikuwa ni Makao Makuu ya Jumuiya toka alipohamia Khalifa Mtukufu wa nne[rh] mnamo mwaka 1984.

Wakati palikuwa na huzuni isiyo shaka miongoni mwa majirani na wakazi wa karibu na Masjid Fazl, furaha kubwa zilikuwa za shukrani kwa Allah kwa kutimiza tena ufunuo wa mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Ahmadiyya uliosema "**tanua makazi yako**" ikibashiri mafanikio ya baadaye ya Jumuiya.

Mbali na msikiti, ofisi kuu mbalimbali za Jumuiya zitakuwepo hapo Islamabad. Ukumbi mkubwa wenye uwezo wa kutumika kwa shughuli mbalimbali na jengo kubwa la makazi pia limejengwa katika eneo hilo.

Wakati ukurasa mmoja wa historia unafikia kikomo, mwingine unafunguka. Chini ya uongozi na mwongozo wa Ukhalifa wa Ahmadiyya, Waahmadiyya wote wanaunganishwa pamoja katika imani yao kwamba zama mpya zitaona muendelezo wa kunawiri na mafanikio ya Jumuiya ya Ahmadiyya.

Anuani Mpya ya Barua kwa Huzur[atba]

Mubarak Mosque,
Sheephatch Lane,
Tilford Surrey,
GU10 2AQ,
United Kingdom

Bustani ya Washairi

MODO

1. Enyi ndugu waungwana, tunakumbushana tena
Wala sio kusemana, moyo wangu unanuna
Nguo zetu za kubana, wala hazina maana
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

2. Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa
Vijana wamedhikika, na zinawabana hasa
Embu anza kukumbuka, usiziwaze anasa
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

3. Mavazi yaliyobana, wanavaa wanawake
Kama waona hiyana, kazana ubadilike
Sisi sote ni vijana, tusizidishe makeke
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

4. Zipo zenye kuchanika, magoti kuonekana
Na pia zenye viraka, zinapendwa na vijana
Miili zimewashika, na kuhema pata shika
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

5. Wanapiga makelele, wanapofundishwa dini
Ujana kuweka mbele, dini ndio kitu gani?
Kazi kupiga misele, mwendo modo ya dukani
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa

6. Chini wanaweka zipu, ili ibane vizuri
Ukiingia upupu, utaipata habari
Waweza baki mtupu, ukiipata ajari
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

7. Mara kuna mpauko, mara kamatia chini
Zunguka huku na huko, kuzunguka madukani
Usijepata anguko, kuanguka hadi chini
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa

8. Nguo yako mekubana, na unashindwa kuhema
Si vizuri we kijana, usiishi kama Kima
Rukia miti kwa sana, kuko wazi huko nyuma
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

9. Na Modo zenye majina, mara Bosi mara Zara
Hakuna kitu hakuna, wanafanya biashara
Vaa nguo za maana, usiulete ubara
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

10. Mnisameheni sana, nimewasema vijana
Bado tutakumbushana, Sisi sote ni vijana
Hata kama mkinuna, na mbavu zikikubana
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
#MMAKONDE MSOMI
kalindimasenior@gmail.com

BURIANI MPENDWA NDUGU REGINARD ABRAHAM MENGI

Huu msiba mzito, Mengi ametuondoka,
Ghafla na kama ndoto, Lulu imetuponyoka
Wamefiliwa watoto,Walemavu kadhalika
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Wamefiwa walemavu, nani ata-w-akumbuka
Kaondoka mshupavu, apendae kila rika
Mengi hakuwa mvivu,kwenye kutoa sadaka
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Kaondoka mwenye moyo, wa huruma hila shaka
Tumebakia wachoyo, vyote sisi twavitaka
Mengi hakuwa na hayo, ndiyo tunamkumbuka
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Yu wapi mfano wako, Zanzibari Tanganyika
Mwenye roho kama yako, kama upo
Atwae pahala pako, tupate kufarijika
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Mimi natoa tambio, kwa dhati sio dhihaka
Kama wapo waje mbio, Tanzania twawataka
Katika hiki kilio, wema wanapotoweka
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Umetuacha kimwili, moyoni tutakumbuka
Wasemavyo waswahili, mwema hafi kama paka
Tunamuomba Jalali, peponi kukupeleka
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Utakumbukwa daima, na watu kila tabaka
Watoto akina mama, na wazee kadhalika
Uloyafanya kwa umma, atakulipa Rabuka
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Buriani ewe Mengi, na njema zako huluka
Umetufanyia mengi,vigumu kuyaandika
Nimetaja ya msingi, mbele yenu kuyaweka
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Na lugha ya Kiswahili, kuilinda hukuchoka
llikua muhimili, kwa taarifa kutoka
Na katika jambo hili, NIPASHE linasifika
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa.

Tamati namalizia,pole nyingi kwa kizuka
Pole enyi familia, sote tunasikitika
Mwenzetu katangulia, nasi siku itafika
Buriani ewe Mengi, Daima utakumbukwa

Said Muhammad Mannoro
Dar es salaam

KIOO

Toka adam zamani, wamanabii ukoo,
Walipata mitihani, wengine kukabwa koo,
Mapambano na shetani, nasi tumeitwa njoo,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Asiyejua ni nani, mi ni vuli na masika,
Nanyesha ulimwenguni, viumbe wa burudika,
Nafarijika moyoni, hata kama nateseka,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Mola hupima imani, mitihani anakupa,
Ajue namna gani, mapenzi unayompa,
Japo huwezi kuwini, bila msada kukupa,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Wote ni sawa thamani, mbele ya weturabbuka,
Waringia kitu gani, na rangi hukujivika,
Tunatengana kwanini, si wote tumeumbika,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Inua macho mbinguni, ninakushika sikio,
Halafu tizama chini, huo ndio mwelekeo,
Utazikwa ardhini, si ajabu hata leo,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Dharau zako za nini, hali yangu wanicheka,
Eti kisa masikini, nguo zimenichanika,
Miye nagonjea chini, mpanda ngazi hushuka,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Ukiona duniani, mtu alivyochafuka,
U idhani
Pengine hajui lini, shidaze zitamtoka,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Jua mawazo kichwani, pindi yakivurugika,
Hutanda giza usoni, pia akili huchoka,
Hata magari huoni, barabara ukivuka,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Najikwae kidoleni, lakini si yako ndimi,
Hata kama uwe nani, usivumishe uvumi,
Ulinde yako lisani, acha kabisa umimi,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Ukiona mtu duni, si kunyoosha kidole,
Tafakari kwa makini, na pia kua mpole,
Tatizo ukibaini, saidia vile vile,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Hii ndo yake mizani, Mola wetu Anapima,
Wakwasi na masikini, kitu gani mtasema,
Majaribu ya fulani, twapimwa wote hekima,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Hapa sasa kituoni, Nang'olo nimemaliza,
Ni Mndumbwe maskani, Tandahimba na kujuza,
Mola wetu Muhisani, naomba Kutuongoza,
Na mimi ndimi kioo, natizamwa duniani.

Mwl. Najat Fakim Said Nang'olo
THE BIG BOSS
AHMADIYYA PAWAGA,
MAGOZI, IRINGA

MAPENZI NA HOFU

Bila mapenzi na hofu, katu huwezi kupona
Hizi njia ni tukufu, kumfikia Rabana
Ukaepuka uchafu, na bahari ya fitina
Mapenzi pamwe na hofu, ni ngao ya kukulinda

Mahmood Hamsin Mubiru
Wa Mamba



RAMADHAN KARIIM

Bodi ya Uhariri inawatakia wasomaji wetu wote wa gazeti hili heri ya mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Allah Atupe kila baraka kupitia mwezi huu.



'Chapakazi'



Katika Kijiji kimoja cha Songambele kulikuwapo na kijana mdogo aitwaye Chapakazi. Kijana huyu alisifika kwa tabia yake ya uvivu na kutosikiliza wakubwa hata wazazi wake. Yeye huwa anasema "nitafanya, sasa nimechoka" katika kila kitu kwenye Maisha yake.

Siku moja wazazi waliamua kukihama Kijiji na kuelekea Kijiji jirani. Waliamuru mtoto wao afue nguo zake zote ili waweze kusafiri siku inayofuata. Mtoto yule alisema "sawa nitafua, sasa nimechoka". Ilipofika asubuhi kijana yule alivaa nguo chafu na zingine kuzisunda kwenye begi. Mama yake alipomuuliza, alisema "nilitaka kufanya, lakini nilichoka".

Safari ilifikia nusu yake na kuanza kupitia msituni takriban maili mbili hivi, ndipo waliweka kituo. Wazazi walikuwa mbali kidogo na mtoto wao. Waliamuru afunge hema ili ajipumzishe, lakini yeye alisema "nitafanya, sasa nimechoka". Alipoletewa chakula, alikisogeza pembeni na akasema "nitakula, sasa nimechoka".



Wazazi walimueleza kuwa ni hatari kulala bila kuwasha moto. Yeye alisema "sawa nitawasha, sasa nimechoka". Alijibanza kando ya gogo kubwa lililopo jirani yake na kuporomosha usingizi mzito.

Ghafla kelele zilisikika msituni na wazazi walipogutuka walielekea kumtazama mtoto wao. Walimuona nyoka mkubwa akitokomea kwenye majani. Chapakazi alikuwa hoi bin taabani huku sumu ikiendelea kutapakaa mwili mzima. Baba yake alitumia mitishamba aliyoichuma pembezoni kumtibia kitambo kidogo Chapakazi akapata ahueni.



Kijana alijiuliza sana alikosea wapi mpaka akakutwa na ajali hiyo!

Kazi

1. Msaidie Chapakazi kutambua makossa yake kwa kuyataja angalau mawili (2).
2. Kwa nini hatutakiwi kuwa kama chapakazi?

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

Quran	Ikhlas	Daku	Dhambi	Masihi
Saumu	Taqwa	Futuru	Wema	AlFazl
Taraweh	Hija	Sihr	Fasiki	Muslih
Ramadhan	Shawwal	Maombi	Mwaminio	Mauud

F	F	U	T	U	R	U	N	B	L	D	B	Q	L	Q
T	T	W	E	M	A	M	N	Z	U	T	Z	X	P	D
T	V	A	Q	F	K	M	A	K	H	W	H	K	N	G
F	F	T	R	N	W	F	A	U	X	N	M	I	R	T
S	L	K	L	A	L	D	N	M	U	D	K	H	J	I
H	Y	B	N	A	W	P	Z	T	M	D	T	M	B	A
A	S	A	U	M	U	E	T	A	Q	W	A	M	T	B
W	M	I	F	M	K	L	H	V	B	Q	A	P	R	N
W	A	X	H	Y	R	F	H	S	H	H	V	T	A	L
A	O	M	Y	R	T	L	A	I	D	X	Q	R	M	Z
L	M	A	B	D	X	L	L	S	L	J	U	R	A	B
V	B	S	W	K	H	S	V	Q	I	Q	Y	W	D	D
C	I	I	N	K	U	B	H	X	R	K	J	Y	H	Q
Q	K	H	I	M	K	H	G	X	J	T	I	C	A	M
J	L	I	X	N	M	W	A	M	I	N	I	O	N	H

CHEMSHA BONGO

Jipime Jinsi Unavyo Ifahamu Qur'an Tukufu

Taja herufi sahihi ya jibu

1. Neno Qur'an Limerudiwa Mara Ngapi ndani ya Qur'an?
A. 67 B. 68 C. 69 D. 70

2. Ni kipi Kinywaji Bora kilichotajwa ndani ya Qur'an?
A.Maji B. Asali C. Juice D. Maziwa

3. Ni ipi Halali Anayo ichukia Allah Subhanah?
A. Hajj B. Talaka C. Ndoa D. Nyama Ya Kondoo.

4. Ni Ipi Sura ndani ya Qur'an Inayojulikana kuwa ni mama wa Qur'an?
A. Baqara B. Fatiha C. Ikhlaas D. Jinni

5. Taja Sura tano ndani ya Qur'an zilizoanza na Alhamdulillah?

6. Ni ipi Sura Inahusiana na sheria ya Ndoa?
A. Talaq B. Mujadala C. Nisa D. Mumtahanah

7. Ni Ipi Sura Inaitwa Shairi la Qur'an
A. Dhuha B. Llayl C. Rahmaan D. Quraish

8. Ni Sura Ipi ndani ya Qur'an Jina la Allah limetajwa kila Aya
A. Ikhlaas B. Mujaadalah C. Jinni D. Mursalaat

9. Ni sura ipi imeelekeza jinsi ya kuumbwa kwa Mwanadamu
A. Hajj B. Hijr C. Hadid D. Humaza

10. Ni upi usiku bora uliotajwa ndani ya Qur'an
A. Qamar B. Qadir C. Najm D. Layl

11. Ni upi Mwezi bora uliotajwa ndani ya Qur'an
A. Rajab B. Sha'aban C. Ramadhan D. Hajj

12. Ni Sura ngapi zinaanza na Bismillahi Rahmani Rahiim
A.116 B. 115 C. 114 D. 113

13. Ni Ipi Sura Kubwa ndani ya Qur'an
A. Yaseen B. Al Ikhlaas C. Al Faatiha D. Masad

14. Ni kipi chakula Bora kilichotajwa ndani ya Qur'an?
A. Pilau B. Biriani C. Asali D. Mkate

15. Aya kubwa Ndani ya Qur'an
A. Ayat Kursiyyu B. Ayat Ddein C. Sab'al Mathaani D. Ayat hijaab

Mahafali ya Wahitimu Jamia Ahmadiyya Yafana

Na **Sheikh Abid Butt**
Mkuu - Jamia Ahmadiyya Tanzania



Kwa fadhila za Allah chuo cha Waalim - yaani Jamia Ahmadiyya kilifanya mahafali ya kuwaaga wahitimu wa mwaka 2018 mnamo siku ya Jumanne tarehe 8.01.2019.

Hafla ilianza majira ya saa 10.30 chini ya Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry ambaye alikuwa mgeni rasmi kwa usomaji wa Qur'an Tukufu na Hafidh Abdul-Rrahman Rundo na kisha kufuatiwa na shairi la Kiurdu lilisomwa na ustaadhi Sultan Amri Junedy.

Taarifa ya mwaka ya chuo kwa lugha ya Kiurdu ilisomwa kwa hadhara kisha kufuatiwa na ya Kiswahili. Taarifa hiyo ilianza kwa kueleza historia fupi ya chuo cha Jamia Ahmadiyya kisha kuwataja wahitimu 8 wa mwaka huo. Taarifa hiyo ilieleza mabadiliko yaliyopitishwa na Huzur^{atba} ya muhula kuanza Januari badala ya Julai.

Taarifa ilisema Chuo kimetoa wanafunzi 3 kwenda nchini Ghana kwa ajili ya masomo ya juu ya ubashiri (Shahada ya Shahid), ambao ni:- Abdul-Azizi Muhammad, Bilal Amir Kaluta, Latif Khalfan Mambo.

Taarifa hiyo ya chuo pia imeeleza namna wanafunzi wanavyohusishwa na kushirikishwa katika mashindano mbalimbali ya kielimu na kimwili, Tarbiyyat, Tabligh, ushiriki katika michango, kazi za kujitolea (Waqar-e-amal), Huduma za kijamii, Huduma za kielimu na chakula katika shule ya msingi ya Ahmadiyya,

Baada ya zoezi la ugawaji zawadi, Amir sahib alitoa nasaha chache kwa wahitimu na wote waliohudhuria. Aliwanasihi wahitimu kuundeleza msingi waliojipatia hapo chuoni na kuufanya nyumba kamili kwa kuitafuta elimu zaidi hadi huko waelekeako.

Pia Amir sahib aliwakumbusha asili ya kazi yao – waqfu, na kuwataka kujiandaa kiakili na pia kuwa wao ni mabalozi wa Jamaat hivyo waiwakilishe sawia watakapopangiwa.

Mahafali hayo yalifungwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Amir Jamaat.



Jamia Ahmadiyya Waadhimisha Siku ya Masihi Aliyeahidiwa^{as}

Na **Sheikh Abid Butt**
Mkuu - Jamia Ahmadiyya Tanzania



Tarehe 23 Machi ni siku muhimu sana katika historia yetu ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ulimwenguni kote kwani ndiyo siku ambayo Hadhrat Masihil Mau'ud^{as} kwa mara ya kwanza alichukua bai'at kutokana na amri ya Allah. Ilikuwa ni tarehe 23 Machi, 1889 ambapo kwa mara ya kwanza tukio hili lilifanyika katika mji wa Ludhiana nchini India ambapo takriban watu 40ra walichukuwa baiat ya Masihi Aliyeahidiwa^{as}. Hivyo tangu siku hiyo kila ifikapo tarehe 23 Machi, kila mwaka matawi yote ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya huadhimisha siku hii adhim. Lengo likiwa ni kufanya tathmini ya kule tutokako, tulipo na mwelekeo wetu lakini pia kuvikumbusha vizazi vyetu kutambua umuhimu wa siku hii.

Jamia Ahmadiyya Tanzania iliadhimisha siku hiyo Jumamosi ya tarehe 23 Machi 2019. Kikao kilianza saa 10.15 chini ya uenyekiti wa Sheikh. Aziz A. Shahzad kwa usomaji wa Qur'an Tukufu na kufuatiwa na shairi la Kiurdu.

Hotuba ya kwanza iliyotolewa na Al-Ustadh Salum Patrick Mhoja ilikuwa na anuani "*Ishara za Kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa^{as}*". Ustadh alieleza jinsi ishara zilivyotimia kwa Hadharat Ahmad^{as}. Kisha alifafanua ishara za kimbingu (kupatwa kwa mwezi na jua) na kufafanua kwa urefu juu ya somo hili.

Baada ya shairi hotuba iliyosema "*Kuendelea kwa Utume*" ilitolewa na Mwl. Abdallah Ramadhan Rundo sahib. Katika hotuba yake Mwalimu aligusia pia maandiko ya Masingasinga kuthibitisha kuendelea kwa Utume. Kisha ilifuata hotuba yenye kichwa kisemacho "*Mapenzi ya Masihi Aliyeahidiwa kwa Allah*" iliyosomwa na Maulana Sheikh Ahmad Daud sahib. Sheikh alitaja matukio kadhaa ya kusisimua na ya kujenga imani yaliyomuacha kila aliyehudhuria kufaidika vya kutosha.

Kisha Naibu Amir Tabligh na Tarbiyat, Sheikh Bakri Kaluta ambaye alikuwa mgeni wa heshima alihutubia hadhara akielezea kuja kwa Mtume^{saw} kwa mara ya pili kwa njia ya burooz. Pia alitoa maelekezo machache juu ya Tabligh, Tarbiyat na mengineyo.

Kaswida ya Kiarabu iliyosomwa na baadhi ya wanafunzi wa Jamia Ahmadiyya ilifuata kabla ya Kaimu Mkuu wa Chuo - Sheikh Ahmad D. Mmoto kutoa nasaha chache kwa wahudhuriaji na maelekezo ya Hadhrat Khalifat ul Masih V^{atba} juu ya shabaha na madhumuni ya maadhimisho ya siku hii. Kisha mgeni rasmi aliombwa kuongoza maombi ya kimya kwa kufunga kikao.

Siku ya Mwana Aliyeahidiwa^{ra} Yaadhimisha Jamia Ahmadiyya

Na **Sheikh Abid Butt**
Mkuu - Jamia Ahmadiyya Tanzania



Kwa baraka za Allah Mwenye Jalali, Jamia Ahmadiyya Tanzania iliadhimisha siku ya Mwana Aliyeahidiwa^{ra} [Yaumul–Muslih Mauud] katika tarehe husika yaani tarehe 20 Februari.

Hafla hiyo ilianza majira ya saa 04:00 asubuhi chini ya mwenyekiti Sheikh Abid M. Bhatti ambaye ni mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya Tanzania.

Kama kawaida, hafla ilianza kwa usomaji wa Qur'ani Tukufu kisha kufuatiwa na shairi la kiurdu pamoja na tafsiri yake halafu ulifuata usomaji wa bishara kumhusu Hadhrat Muslih Mauud^{ra} na Bw. Ramadhani Abdallah Witika

Baada ya hapo ilifuata hotuba yenye anwani isemavyo "*Jinsi Bishara Kumhusu Muslih Mauud Zilivyotimia kwa Hadhrat Mirza Bashirud-din Mahmood Ahmad^{ra}*". Mwalimu Mwalim Abdallah Ramadhani Rundo alifafanua mada yake kwa aya za Qurani tukufu, hadithi mbalimbali za Mtume mtukufu^{saw} ikiwemo hadithi ile maarufu isemayo, Masihi na Mahdi^{as} ataoa na atazaa. Pia mwalim alinukuu maelezo ya mawalii na wanazuoni wa zamani kuithibitisha mada hii. Kisha ilifuata hotuba isemayo "*Baadhi ya Kazi Alizofanya Hadhrat Muslih Mauud*" iliyotolewa na Bw. Ramadhani A. Mkieti. Alielezea kazi adhim ya kuandika Tafsir Kabiir, kuandaa wabashiri na kuwatuma katika nchi mbalimbali duniani, kufungua vituo katika nchi mbalimbali, kuanzisha Majlis Shura [kikao cha mashauriano], kuanzisha mpango wa Tahrik Jadid na Waqf Jadid, kuanzisha tanzim [makundi ya rika na jinsia] mbalimbali katika Jumuiya, nk.

Baada ya hotuba hiyo, lilifuata shairi la Kiswahili kisha ikafuata hotuba yenye anuani isemayo "*Atajazwa na Elimu ya Ndani na ya Dhahir*" iliyotolewa na Sheikh Shabani Athumani Shunda. Sheikh alisema, ingawa mwana huyu mtukufu hakuwa na maendeleo mazuri darasani, lakini hali yake ya baadae ilithibitisha kuwa alijazwa na Mwenyezi Mungu elimu maalum.

Baada ya hotuba hiyo iliyoamsha ari na hisia za wasikilizaji, zilifuata nasaha chache kutoka kwa mgeni rasmi ambaye pia ni Mbashiri wa Jumuiya katika mkoa wa Mbeya – Sheikh Kareem-ud-din Shams. Mgeni rasmi alielezea wasifu na sira ya Hadhrat Muslih Mau`ud^{ra} na matukio mbalimbali ya kusisimua yaliyojiri katika zama za Ukhalifa wake. Mwisho aliwataka wasikilizaji kuongeza imani na taqwa kupitia maisha, khulka njema na ikhlasi ya Mwana Aliyeahidiwa^{ra}.

Baada ya nasaha, Mkuu wa Chuo ambaye pia alikuwa mwenyekiti wa hafla hiyo alitoa shukrani kwa wahudhuriaji na kumtaka mgeni rasmi kuongoza maombi ya kimyakimya ili kufunga kikao.

MATUKIO KATIKA PICHA



Khalifa mtukufu akiongoza ibada katika Masjid Mubarak baada ya kuwasili Islamabad



Khalifa mtukufu akiongoza maombi ya kimya kabla ya safari ya kuelekea Islamabad





Ufunguzi wa Madarasa manne ya Shule ya Msingi Ahmadiyya Morogoro



Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania akihutubia kikao cha maadhimisho ya Siku ya mwana Aliyeahidiwa katika ukumbi wa Jamia Ahmadiyya Tanzania



Naibu Amir Tabligh na Tarbiyyat akihutubia kikao cha maadhimisho ya Siku ya Masihi Aliyeahidiwa katika ukumbi wa Jamia Ahmadiyya Tanzania







Matukio ya Ijtimaa ya Waqf -e-Nau nchini Tanzania mwaka 2019

Historia ya Mzee Mwishehe Juma

Na **Familia ya Marehemu**

Dain Mzee Mwishehe Juma alizaliwa mwaka 1934 katika kijiji cha Lung'ara kata ya Kinole. Baba yake anaitwa Juma Waziri Kiosi Mgulo bin Timbwi bin Mkondo wa maji bin Chawila. Mama yake aliitwa Bi. Mwajabu Binti Mwishehe. Alikuwa ni Ahmadiyya wa kwanza kujiunga kijiji cha kinole Tarafa ya Mkuyuni.

Kuzaliwa Kwake na Jina Lake.

Miezi michache kabla ya kuzaliwa kwa Dain Ilallah huyu mama yake (Bi. Mwajabu Binti Mwishehe) alijiona kwenye njozi kwamba; "yupo katika chumba fulani akiwa kwenye harakati za kujifungua. Kisha akaona kwamba amejifungua mtoto wa kiume, kisha katika hali hiyo hiyo ya njozi akasikia sauti ya baba yake kutoka nje akiuliza; "mbona nasikia sauti humo ndani?" Mama huyo akamjibu baba yake njozini; "kuna mdogo wako humu ndani" (yaani mjukuu wake). Baba yake akamjibu; "ikiwa kuna mdogo wangu, basi aitwe Mwishehe" na alisisitiza hivyo mara tatu humo kwenye njozi.

Alipoamka usingizini alimsimulia mumewe mzee Juma Waziri Kiosi. Ndipo baada ya miezi michache kupita, yaani mwanzoni mwa mwaka 1934 mama huyo (Mwajabu binti Mwishehe) alipata kujifungua mtoto wa kiume na akapewa jina lilelile la Mwishehe kulingana na njozi yake.

Elimu Yake

Mzee Mwinshehe alipata elimu ya dini tu. Mwaka 1949 alisoma kidogo elimu ya dini kwa Sheikh Hassan Nassoro. Baba yake yaani Mzee Juma Waziri Mwinyipanda alikuwa na shauku kubwa kwamba kijana wake apate elimu ya kutosha juu ya dini ili shughuli za kifamilia zinazohusu dini hususani kwa wakati ule mambo ya dini yaliyojulikana zaidi yalikuwa ni usomaji wa maulidi, hitima, tatu, arobaini na hata usomaji wa 'Ahlul Badr' n.k.w awe anazifanya yeye bila ya kusumbuka kuwaita masheikh. Hivyo mwaka 1950 akampeleka Unguja kwa shabaha hiyo. Aliendelea kusoma huko Zanzibar kwa muda wa miaka mitano (1950 – 1955). Akiwa huko alisoma vitabu mbalimbali vya dini kama vile Hidaayat-ul-atfaal, Ruhul-ibada, Nuz-hatul Majaalis, Safinatu ibn majaa na vingine vingi. Mwenyewe aliwahi kuhadithia kuwa; wakati anaelekea mwisho wa masomo yake huko Unguja, alipata nasaha kutoka kwa masheikh wawili tofauti. Sheikh wa kwanza alimwambia yeye pamoja na wenzake kuwa, "Ninyi vijana mnasomea dini ili muwe imara na makini kwa sababu kuna mpotoshaji mkubwa wa dini anakuja, na mpotoshaji huyo ni hatari sana kwa sababu anafanana sana na Uislamu." Naye Sheikh wa pili alimwambia wakati alipoenda kumuaga baada ya kuhitimu masomo yake kuwa; "mimi nawahurumieni sana nyinyi vijana mliosomea dini kwa sababu masheikh wenu hawatawapendeni." Ingawa alishtushwa sana na kauli hii lakini hakuthubutu kuhoji ili asije kuonekana kuwa ni mtomvu wa nidhamu.

Alivyorudi kutoka Unguja mnamo mwaka 1956, alirudi nyumbani baada ya kuhitimu masomo yake, na akawa anafundisha tofauti na mtizamo wa Masheikh wakubwa wa eneo lile kama khitima na hakika.

Jambo hili lilizua mgogoro baina yake na Masheikh na kupelekea kupishana na Sheikh mkuu wa tarafa ya Mkuyuni wa wakati huo Sheikh Chang'walo. Masheikh hao waliombwa ushahidi wa masuala wanayoitakidi kutoka kwenye Qur'an Tukufu bila kufanikisha na kuishia kumtoa ufahamu Mzee Mwinshehe, jambo lililompa hofu baba yake huenda mwanae akarogwa.

Moja kati ya siku alizowahitaji Masheikh kuleta ushahidi wa khitima katika Qur'an Tukufu kuwadia, alipatwa na hofu katika kukabiliana nao. Rafiki yake mmoja aitwae Mustafa Abd-ul-rahmaan alimpa ushauri wa kupata msaada kutoka kwa Waahmadiyya naye bila ajizi akafunga safari hadi Morogoro Mjini na kupokelewa na Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima.

Mzee Mwishehe aliomba kupatiwa silaha tu ya kupambania badala ya kupewa jeshi zima. Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima alimfundisha na kumpatia aya tano (ikiwemo 63:10-12) na kumsihi kutotoka nje ya boma la Qur'an Tukufu katika mnakasha huo.

Wanakijiji ambao walidhani amekimbia mjadala walifurahia mrejeo wake kwani mjadala ulitangazwa sana kijijini. Tarehe ilipowadia palikusanyika wanakijiji wengi ambao sehemu yao kubwa walikuwa Waislam msikitini kwa Sheikh Chang'waro kushuhudia. Watu walistaajabu kumuona Mzee Mwinshehe mikono mitupu na kuhisi atashindwa kiurahisi baada ya kudai kwamba kitabu kipo kwa Sheikh Chang'waro.

Mjadala ulipoanza Mzee Mwishehe akatoa muhtasari kwa kusema, katika masomo yake aliyosoma hakuona aya inayoamuru habari za Khitima na ya kwamba Sheikh amemuahidi kumuonesha aya zinazohusu somo hili ili ajifunze kutoka kwake. Sheikh akaagiza aletewe Qur`an Tukufu na kuanza kuifungua tangu mwanzo hadi mwisho na kurudia mara tatu bila ya kupata aya inayokusudiwa, ndipo umati wa watu uliokusanyika ukapigwa na butwaa na kung`amua kuwa kumbe maelezo ya yule aliyeonekana kuwa ni kijana mdogo huenda yana ukweli. Sheikh akakasirika na kwenda kushitaki mahakamani kuwa amefanyiwa vurugu msikitini kwake. Kesi hiyo lifutiliwa mbali na mahakama.

Basi hapo Mzee Mwishehe Juma akapata nguvu ya kuhubiri uharamu wa Khitima na njia sahihi ya kufanya hakika. Ndipo masheikh wakawa wanamwita kuwa ni "Qadiani", jina ambalo lilimuudhi sana kwani alipokuwa masomoni Unguja aliambiwa "Qadiani" anakuja, naye ni mpotoshaji mkubwa wa dini ya kiislamu. Akafunga safari ya kwenda Morogoro mjini kwa makusudio mawili, kwanza kumpa mwalimu wake Sheikh Swaleh taarifa ya matokeo ya mjadala kuwa ameshinda, na pili kumweleza tatizo lililojitokeza la yeye kuitwa "Qadiani".

Sheikh Swaleh Mbaruku akamtuliza na kumweleza kirefu juu ya neno Qadiani na tafsiri sahihi na mafundisho ya sahihi yaliyoletwa na Imam wa zama hizi. Na kuambiwa kuwa atakaekufa bila ya kumjua imamu wa zama atakuwa amekufa kifo cha kijinga.

Baada ya maelezo hayo, Sheikh Swaleh Mbaruku akamchukua mgeni wake na kumpeleka kwa Sheikh Jamil-Ur-Rahman Rafiq sahib ambaye alikua ndiye mbashiri wa mkoa wa Morogoro wakati huo na baada ya mahojiano mafupi akajiunga na Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya.

Baada ya kujiunga na kuhubiria majirani na ndugu, alifanikiwa kuwashawishi Mzee Idd Suleiman Juma na mkewe Bi. Halima Juma ambao walitembea kilometa arobaini hadi Morogoro Mjini kujaza Bai'at.

Baada ya hapo aliendelea kuhubiri kwa jazba kubwa, upinzani ulikuwa mkali sana na hasa sokoni Mkuyuni ambapo Wanajumuiya walikuwa wakizomewa, kutupiwa majani ya ndizi na hata kutishiwa maisha. Lakini kumbe wachache wenye ikhlasi walikuwa wakifuatilia kwa makini sana na hatimaye polepole Wanajumuiya wakaongezeka. Miongoni mwa wale waliojiunga wakati huo ni kaka yake Mzee Muhammed Juma, shemeji wa Mzee Iddi Suleiman- Mzee Ramdhani Juma Rundo, Mzee Said kondo na hatimaye Mzee Jaffar Ismail Msesemele [hawa wote wameshatangulia mbele ya haki, Allah awarehemu] na Mzee Shaban Jaka ambaye yu hai. Wanajumuiya hao walisimama imara kweli kweli na Jumuiya ikaimarika hasa Mkuyuni na wabashiri wa Mkoa wakawa wanawatembelea, na kati yao ni Maulana Sheikh Ashraf. Nakumbuka mwaka 1991 Al-hajj Sheikh Bakri Kaluta [Naib Amir Tabligh na Tarbiyyat] akiwa mbashiri wa mkoa wa Morogoro wakati huo alipotembelea Jamaat ya Mkuyuni alivutiwa sana na hamasa na jazba ya Wanajamaat hao wa Mkuyuni katika kudumisha mila za Kiislam hususan kufuata maamkizi ya Kiislam ya 'assalaam alaikum' mpaka watoto wadogo na kupiga vita maamkizi ya 'shikamoo' ambayo yalitamalaki mno siku hizo.

Licha ya upinzani mkali alioupata, aliendelea na

Endelea uk 11

Historia ya Mzee Mwishehe Juma

Inatoka uk 10

mahubiri kwa jazba hasa katika soko la Mkuyuni na hatimaye kuwatia kwenye Safina ya Nuhu wa zama hizi Mzee Muhammed Juma, Mzee Ramadhani Juma Rundo, Mzee Said Kondo, Mzee Jaffar Ismail Msesemele na Mzee Shaban Jaka.

Shauku Yake Juu ya Kuitumikia Jumuiya

Tangu ajiunge na Jumuiya shauku na hamu yake kubwa ilikuwa ni kuitumikia Jumuiya hii ya Allah.

Mzee mwishehe alipenda sana kulitumikia jeshi tangu udogoni, lakini akaishia kulitumikia jeshi hasa la Masihi wa zama.

Kujitolea maisha yake kumsaidia Imam wa Zama Zake.

Alishawahi kuweka nadhiri kwa Allah kuwa ataitumikia dini yake endapo Atamshusha Isa bin Mariam kuja kunusuru zama hizi. Kwa kutimiziwa hilo, mara kwa mara aliirejea kauli hii akiongea na Mwl Yusuf; "Yusufu unajua kuwa mimi nilimuahidi Mola wangu kumsaidia endapo Yeye Atamteremsha Nabii Issa bin Mariam kutoka mbinguni, hivyo nina deni la kutekeleza jukumu hili bila udhuru wowote"

Ajitolea Kuwa Mpishi Kwenye Mikutano ya Jalsa salana.

Dain Mwishehe Juma alikuwa makini kuangalia fursa zilizo ndani ya uwezo wake ili azitumie kikamilifu kumtumikia Mola wake. Jambo la kwanza alipobaini kwenye Jamaat kuna utaratibu wa mikutano ya mwaka (Jalsa Salana) yeye alihakikisha anahudhuria kwenye Jalsa Salana hizo bila kukosa tena ikibidi na watoto zake wote. Kwenye Jalsa Salana yeye alibaini fursa ya kujitolea kule jikoni, wakati wake ilikuwa ni desturi yake kuhakikisha mara akifika kwenye mkutano basi anatumia muda wake wote kule jikoni katika maisha yake yote.

Ajitolea Kuwa Mpishi wa Jamia Ahmadiyya –Morogoro

Kuna wakati chuo chetu cha wabashiri kule Jamia Ahmadiyya Morogoro palikuwa shida ya kumpata mpishi, kwani sawa na hali ya Jamaat wakati huo kifedha hahikuweza kumuajiri mpishi maalum kwa ajili ya kuwapikia wanafunzi. Hivyo mnamo mwaka 1984 yeye aliichangamkia fursa hiyo na akajitolea kuwa mpishi wa chuo bila malipo yoyote. Alifanya kazi hiyo kwa muda wa miaka takribani mitatu kutoka 1984 – 1987.

Matukio ya Kuongeza Imani kwa Kutawakkali Kwake Juu Ya Allah

Hapo Jamia Ahmadiyya alipokuwa anajitolea palikuwa na vijana wake watatu ambao walikuwa wanasoma na aliwasisitizia kuendelea na masomo na kuacha kujishughulisha na utafutaji dunia. Huko nyumbani kwake aliwaacha watoto wengine pamoja na mama yao. Kwa hali aliyoiacha nyumbani kwake, msituni juu ya milima ya Uluguru ilikuwa ni kama dhabihu ya Hadhrat Hajra na mwanae Ismail kule jangwani walikoachwa na baba yao Hadhrat Ibrahim (as) kwa ajili ya kutekeleza agizo la Mola wake Mtukufu.

Ajitolea Eneo Lake Kujenga Msikiti.

Ikumbukwe kuwa maisha ya familia yetu yalikuwa ni huko msituni juu ya milima. Hali ya nyumba yetu ni duni sana. Ni nyumba ya nyasi isiyo na wasaa wa kutosha. Kwa shughuli za ibada. Hata hivyo nakumba nyumba yetu ilikuwa na vyumba vinne. Kati ya hivyo baba alikitenga chumba kimoja kwa shughuli za ibada. Nakumbuka tulikuwa tunakiita chumba kile; "Chumba cha kusalia". Katika mazingira yale duni baba hakuwa anaridhishwa na kitu kimoja nacho ni kukosa mahala pazuri pa kusalia. Hivyo alifanya maombi kwa Mola wake ili Ajaalie mahali pazuri pa kusalia. Na huo ukawa ndio msingi wa upatikanaji wa msikiti wa kwanza wa Jamaat za Mkuyuni uliojengwa kwenye kitongoji kidogo cha Mkami juu ya milima ya Uluguru. Msikiti ulijengwa kwa kujitoa sana maana vifaa mbalimbali vilitoka chini ya mlima umbali takriban kilometa 5.

Ajitolea Kufanya Mahubiri Pamoja na Masheikh Mbalimbali.

Wakati wa uhai wake alishirikiana kwa shauku sana na Masheikh mbalimbali hususani waliokuwa wasimamizi wa Mkoa wa Morogoro na hivyo alitembelea maeneo mbalimbali ya mkoa wa Morogoro kwa ajili ya mahubiri mathalani Kilosa, Ifakara, Turiani, Duthumi, Mikese – ambako aliweza kufungua Jamaat ya Lukonde na Kinonko, n.k katika harakati hizo Masheikh alioweza kushirikiana nao ni pamoja na Maulana Jamil-Ur- Rahman Rafique, Maulana Inayatullah Ahmad, Maulana Maqboor Rafiq, Maulana Abdulrahman Khan (wa Guyana), Maulana Ahmad Shad, Maulana Waseem Ahmad Khan na Maulana Asif Mahmood Butt hao wote ni Masheikh wa Jamaat ambao kwa namna moja ama nyingine walifanya kazi katika Mkoa wa Morogoro.

Ateuliwa Kupeleka Qur'an Tukufu Kwenye Vilele Vya Mlima Kilimanjaro.

Katika madhimisho ya sherehe za Karne ya Jamaat mwaka 1988 kulikuwa shughuli mbalimbali zilipangwa kutekelezwa. Moja ilikuwa ni kupeleka Qur'an Tukufu kwenye vilele mbalimbali vya Mlima wa Kilimanjaro. Hivyo pamoja naye wajumbe wengine walioteuliwa kuwemo kwenye msafara huo walikuwa ni Bw. Shuwaib Mohammed Juma wa Mkuyuni na Bw. Athumani Ungele wa Mtwara. Baada ya kurudi safari yake hiyo aliwahi kunieleza kuwa mazingira yote aliyoyaona huko aliwahi kuyaona mapema kwenye njozi muda mrefu uliopita.

Ateuliwa Rasmi Kuwa Dain Ilallah Wa Jamaat.

Kati ya mwaka 1998 na 1999 ndipo chini ya Sheikh Abdulrahman Khan wa Guyana baba aliombwa awe mtumishi wa moja kwa moja wa Jamaat kama Dain Ilallah — wadhifa ambao aliutumikia kwa nguvu zake zote mpaka alipoaga dunia tarehe 13 Machi 2019.

Nidhamu Yake Katika Jama`at

Pamoja na umri wake kuwa mkubwa lakini daima aliwaheshimu na kuwapenda sana waalimu na wabashiri. Nakumbuka hata kabla hajawa Daian Ilallah alikuwa akiiitwa mara kwa mara na Mbashiri wa mkoa kufanya kazi mbalimbali ikiwemo mahubiri, kutembelea matawi n.k. Kuna wakati alikuwa akikaaa nyumbani wiki moja tu na kuitwa tena na alitii wito bila ya kusita huku akisema; "hii ndio sifa ya mwaminio" yaani kusikia na kutii.

Alikuwa akituhimiza kufanya maandalizi ya kurudi chuoni siku tatu kabla ya tarehe ya ufunguzi na kukemea tabia ya kuiga kuchelewa kuripoti.

Kujitolea kifedha:

Marehemu Alikuwa Musi na aliwahimiza wengine kwa nguvu zote kujiunga katika mpango wa Wasia.

Alikuwa akiukata mchango kwa mara ya pili kutoka kwenye posho yake ambayo imeshakatiwa tayari ili tu kupata ile ladha ya kutoa. Licha ya ugonjwa wake, lakini alikatia mchango fedha zote alizokuwa akipokea kutoka kwa watu mbalimbali waliokuwa wakija kumuona.

Maradhi na Kifo Chake

Marehemu Mzee Mwishehe alipatwa na presha ya kupanda tangu Februari 2015 na ilipofikia Januari 2019 maradhi hayo yalizidi na kumdhoofisha na ikawa ajali yake ya kumkutanisha na Mola wake siku ya Jumatano ya tarehe 13-03-2019 majira ya saa 4:00 usiku. INNA LILAAHI WA INNA ILAIH RAAJ`UUN.

Allah Amjazie penye mapungufu, Amghofirie na Amjaalie makazi mema peponi. Amin.

Mazishi Yake.

Wanafamilia tulisafirisha mwili kutoka Mkuyuni, Morogoro vijijini kuja kuuzika Dar es salaam kwenye makaburi ya Musi (Watu waliojiunga na mpango wa Wasia) hapo Temeke Wailesi. Wanakijiji walishangazwa na suala hili maana imezoeleka kuona kwamba watu wakifariki mijini na huzikwa katika vijiji vyao lakini Mzee Mwishehe amefariki Mkuyuni na kuzikwa Dar es salaam hadi kupelekea wengine kusema; "Maqadiani sio wa kuchezea, wamemchukua mtu wao kwenda kumzika Dar es salaam!!"

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

SHA'B. - RAMADHAN 1439 AH | MEI 2019 | HIJRAT 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Mtu anayefunga Ramadhani, kisha akafunga siku sita za mwezi Shawwaal (Mfunguo mosi), yeye ni kama amefunga mwaka mzima" (Muslim).

Ramadhan ni Mwezi wa Taqwa - Khalifa wa Islam

Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin^{atba} alisoma aya 184 ya sura Al Baqarah:

Tafsiri: *Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu.* (2:184)

Hudhur^{atba} alisema: Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu na baraka Zake, mwaka huu pia sisi tumebahatika kushuhudia mwezi mtukufu wa Ramadhan. Katika mwezi huu Waislamu wengi duniani kote wanahudhuria misikitini kusali na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Aya hi niliyoisoma mbele yenu inatukumbusha ya kwamba kusudio kuu la kufunga saumu ni kupata kumcha Mungu. Nalo lilikuwa kusudio la kuwalazimisha watu wa kabla ya Uislamu.

Sisi Waahmadiya tuna jukumu kubwa la kufahamu na kuelewa falsafa ya saumu na inabidi tujitahidi kuyapata yale unayolenga mwezi huu mtukufu, yaani kupata Taqwa na kuzidi pia.

Kuna aya zingine zinatuonesha umuhimu wa mwezi wa Ramadhan na kiini cha Aya zote hizi ni kufanya bidii ili tupate kumcha Mungu. Mwezi huu haswa tunatakiwa kujitahidi katika kufuata mafundisho ya Mwenyezi Mungu na kumuabudu ipasavyo ili mambo haya yawe sehemu ya maisha yetu mazima.

Katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhan tutakapofanya jitihada ya kuupata ucha Mungu, tutakuwa tumepata jazba ya kufanya ibada zaidi na kujiepusha na mambo mabaya. Na tunapokuwa sisi hatujiepushi na mambo hayo mabaya basi tutakuwa hatutimizi kusudio la ibada ya saumu. Ikiwa katika saumu mtu atakuwa na tabia ya kiburi, ubinafsi na kujipendelea basi tabia hii haitakuwa ya kiucha Mungu. Na vile vile mtu baado kama atakuwa na tabia ya kugombana na kutukana basi hii pia haitakuwa tabia ya kiucha Mungu.

Hudhur^{atba} alieleza: Baadhi ya watu hufunga saumu kwa ajili ya kujionesha tu. Kijana mmoja alikuwa anaeleza katika kipindi kimoja Cha TV ya kwamba yeye alikuwa anakula daku na jioni alikuwa anafuturu kwa futari za aina mbalimbali lakini haya yote aliyafanya kwa sababu ya msukumo wa jamii yake iliyokuwa na kawaida ya kufunga saumu lakini wakati wa mchana alikula kama kawaida. Kijana huyu akaongeza ya kwamba hivi hivi ndivyo wanavyofanya vijana wengi wengine.

Hudhur^{atba} akakazia ya kwamba hii ndiyo hali halisi ya saumu ya baadhi ya watu yaani mtu kama ameacha kula na kunywa kutwa nzima bila ya kujali Sala wala kufuata yale yaliyoamrishwa, na yale yaliyokatazwa, basi lile kusudio la saumu halitafikiwa.

Sisi Waahmadiya tuna jukumu kubwa mabegani mwetu la kutekeleza ibada hii ya saumu sawasawa kwa kuzingatia ucha Mungu ni nini na kuna njia gani ya kuupata.



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akihutubia Ijumaa katika msikiti wa Baitul Futuh uliopo jijini London nchini Uingereza ambapo hotuba yake hurushwa mubashara kupitia satelaiti duniani kote kupitia MTA.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} katika sehemu mbalimbali ameeleza kuhusiana na ibada ya saumu na jinsi ya kupata ucha Mungu.

Mwaminio wa kweli anatakiwa kulifanya kila jambo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu na hii ndiyo tofauti pekee kati ya mwaminio na kafiri.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} alisema: Kama Kuna Jumuiya yoyote isiyokuwa na Taqwa mbele ya Mwenyezi Mungu, msaada Wake hautakuwa pamoja nayo. Taqwa ndiyo msingi wa mafundisho ya vitabu vyote vitakatifu vikiwemo Torati na Injili. Mwenyezi Mungu katika neno hili moja tu la Taqwa Amejumuisha matakwa yake na radhi yake yote.

Kisha akasema: "Kama mnataka maombi yenu yapokelewe basi tembeeni katika msingi wa Taqwa, kwa sababu ndiyo msingi wa sheria zote za Quran. Madaraja ya kupata ucha Mungu ni mengi lakini kama mtu akijitahidi, huweza kupata madaraja ya mwanzo na anapoendelea kupita katika madaraja hayo kwa nia safi basi hufikia madaraja ya juu zaidi. Mwenyezi Mungu Anasema: *Kwa yakini, Allah Huwakubalia wale walio wacha Mungu tu* (5:28). Yaani hii ni ahadi yake, naye hafanyi kinyume na ahadi zake. Basi hili ni sharti la kukubaliwa maombi. Yule anayeghafilika na tena anataka maombi yake yapokelewe, basi ni mtu mjinga.

Kwa hiyo kila mmoja katika Jumuiya yetu anatakiwa atembee katika njia halisi ya ucha Mungu ili tuweze kupata ladha ya kupokelewa kwa maombi yetu na imani iongezeke.

Kisha akasema tena: Kwa ajili ya wacha Mungu na watawa kuna ahadi nyingi. Je Kuna ahadi iliyo nzuri zaidi kuliko hii ya kwamba Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye atakuwa mlinzi na msaidizi wake? Watu wale wanaodai kuwa karibu na Mungu wakati hawana Taqwa na badala yake wanaishi katika maisha ya ufisadi na ufasiki, wao ni waongo.

Allah Anasema: *Kwa yakini Allah Yu pamoja na wale wamchao na wale wafanyao wema* (16:129), yaani Anawasaidia. Kumbukeni msaada wake hawaupati walio wachafu na mafasiki.

Hadhrat Khalifa mtukufu^{atba} alisema: Sisi tunatikiwa kusoma sana aya hii na kuizingatia:

Yule amchaye Mungu, Humjaalia njia ya kuokoka na Humpa riziki kutoka mahali asipopategemea. (At-Talaaq 65:3-4)

Kisha Masihi Aliyeahidiwa^{as} akaendelea kusema: Mcha Mungu katika nyumba yake ndogo hupata furaha ya kweli ambayo mtu wa dunia mwenye tamaa hawezi kuipata hata katika kasri la kifahari. Kadri mtu anavyozidi kuipata dunia ndivyo anavyozidi kupata mitihani. Basi kumbukeni furaha haswa haipati anayetafuta dunia. Msifikiri kuwa wingi wa mali, nguo za fahari na vyakula vizuri vinaweza kuwa sababu ya furaha ya kweli. Haiwezekani. Bali msingi wa furaha ya kweli haswa ni ucha Mungu.

Taqwa ina matawi mengi yaliyoenea kama nyuzi za wavu wa buibui. Na sehemu iliyo dhaifu zaidi inahusiana na ulimi. Wakati mwingine mtu husema jambo akiwa amesahau Taqwa. Bwana mmoja mcha Mungu alikaribishwa nyumbani kwa mtu wa dunia. Ulipofika muda wa chakula, mwenyeji akamwagiza mtumishi wake alete sahani aliyoinunua wakati wa Hija ya kwanza. Alipoileta akamwagiza kuleta sahani nyingine aliyoinunua wakati wa Hija ya pili. Nayo alipoileta akamtuma tena kuleta sahani nyingine ya tatu aliyoinunua wakati wa Hija ya tatu. Yule bwana mgeni akasena: Wewe ni mtu wa kuhurumiwa sana. Kwa usemi wako huu umeharibu Hija zako zote tatu. Kusudio lako la hayo yote ni kutangaza kuwa wewe umewahi kuhiji mara tatu. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Amefundisha ulimi unatakiwa utumike kwa uangalifu mkubwa.

Hudhur^{atba} akasema: Katika kufunga saumu mtu anatakiwa azidi katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu na apunguze kuzungumza mambo yasiyofaa ili kupata kusudio la saumu na kuufikia ucha Mungu.

Hadharat Masihi Aliyeahidiwa^{as} anasema: Wema una sehemu mbili, moja ni faradhi na nyingine ni ya nafal. Faradhi ni ile ambayo ni ya lazima kama vile mtu anavyolipa deni au malipo ya wema ni kufanya wema. Pamoja na faradhi hizi, kila wema una nafali zake. Yaani kufanya wema zaidi ya ule anaostahiki mtu. Yaani malipo ya hisani ni kutenda hisani zaidi ya ile iliyofanywa. Mambo haya ni baadhi ya yale yanayozikamilisha faradhi. Imesimuliwa katika hadithi ya kwamba vitendo vya faradhi vya Mawalii wa Mwenyezi Mungu hukamilishwa na nafali zao. Yaani zaidi ya kutoa zaka hutoa sadaka na michango mingine pia. Mwenyezji Mungu mwenyewe Anakuwa rafiki wa watu kama hawa. Mwenyezji mungu Anasema, urafiki wake na mtu unafikia hatua ya kwamba Yeye mwenyewe Anakuwa mkono, mguu na hata ulimi wake anaozungumizia.

Kisha Hadharat Masihi Aliyeahidiwa^{as} alisema: Tabia ya mwaminio wa kweli ni hii ya kwamba, kila anapopata mafanikio anahisi haya na humtukuza Mwenyezi Mungu kwa sababu Yeye ndiye Aliyetoa fadhili zake na ndivyo anavyoendelea kusonga mbele. Naye husimama imara katika kila mtihani anaopata. Kwa dhahiri mafanikio ya mwaminio na kafiri yanashabihiana lakini mafanikio ya kafiri yanampeleka kwenye kiza kwa sababu Yeye haelekei kwa Mwenyezi Mungu bali anazifanya juhudi, akili na uwezo wake kuwa Mungu. Upande mwingine mwaminio huelekeza haya yote kwa Mwenyezi Mungu na kujenga naye uhusiano mpya. Hivyo kila anapopata mafanikio anazidi katika ukaribu Naye na kupata mabadiliko mema mapya.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} alisema: Mwenyezi Mungu Hutengeneza orodha ya vitendo vya mwanadamu basi mtu anatakiwa aweke orodha ya vitendo vyake vya kila siku na atafakari kwa kiasi gani amezidi katika kutenda vitendo vizuri. Hali yake ya leo haitakiwi ilingane na ile ya jana. Yule ambaye hesabu ya vitendo vyake vya leo inalingana na ile ya jana bila shaka amepata hasara. Lazima kila siku vitendo vyake vyema viongezeke. Kama mtu ni mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na kuwa na yakini naye, basi yeye hataangamia bali maelfu ya watu wanaokoka na mabalaa mengi kwa sababu yake.

Mwenyezji Mungu Atujaalie katika mwezi huu wa Ramadhani tufunge saumu kwa kuzingatia Taqwa nao uwe wenye baraka tele. Hususan maombi makhsus yanatakiwa kwa ajili ya nchi ya Pakistan kwa sababu hali inazidi kuwa mbaya. Mwenyezji Mungu Awahurumie Waislamu wote na Awajaalie akili ya kumtambua Imamu wa zama. Kila siku duniani kuna habari ya kutokea kwa Vita Kuu. Mataifa makubwa yanaelekea kwenye vita hivyo. Mwenyezji Mungu Awanusuru Waislamu wote na hususan Waahmadiya kutokana na athari zake mbaya na pia awaokoe wanadamu wengine.

Mwenyezji Mungu Ajaalie hali ya watu wamtambue Yeye ili wanusurike na maangamio ya Vita hivyo. Aamin.

Ifahamu Miiko ya Saumu uk. 2